# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

Anwani ya Simu: **"TUME"**
**DODOMA**
**Nambari ya Simu:** 0738 166 703
0733 005 974
**Barua pepe:** secretary@psc.go.tz
***Tovuti:*** *www.psc.go.tz*

Tume ya Utumishi wa Umma,
Jengo la Chimwaga (UDOM),
Ghorofa ya 2,
2 Barabara ya UDOM,
S.L.P. 1074,
**40405 DODOMA.**

## TAARIFA KWA UMMA

Tume ya Utumishi wa Umma (TUU) ilifanya Mkutano wake wa pili kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kuanzia tarehe 01/12/2025 hadi tarehe 19/12/2025 kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Mahakama Jumuishi ya Tanzania uliopo katika Manispaa ya Morogoro chini ya Mwenyekiti wa Tume **Jaji (Mst.) Hamisa H. Kalombola** na kupitia, kujadili na kuamua Rufaa na Malalamiko ya Watumishi wa Umma yaliyowasilishwa mbele yake.

Katika Mkutano huo, jumla ya Rufaa na Malalamiko **88** yaliwasilishwa na kutolewa uamuzi katika mchanganuo ufuatao:-

(i) Rufaa **63**

(ii) Malalamiko **25**

Katika Rufaa zilizowasilishwa na kuamuliwa makosa yalioonekana kutendwa zaidi na Watumishi wa Umma ni pamoja na:-

(i) Utoro kazini;

(ii) Wizi wa mali za umma na rushwa;

(iii) Kughushi vyeti na kutoa taarifa za uongo;

(iv) Kukiuka Maadili ya Utumishi wa Umma;

(v) Uzembe uliosababisha hasara kwa Serikali; na

(vi) Uzembe wa kushindwa kutekeleza majukumu ipasavyo.

Aidha, kwa upande wa malalamiko, malalamiko mengi yaliyowasilishwa na kuamuliwa na Tume yalihusu kupinga mambo yafuatayo:-

(i) Watumishi kutolipwa stahili zao na Waajiri wao ikiwemo mishahara, stahili za uhamisho na posho mbali mbali za kisheria zinazotokana na kutekeleza majukumu yao;

(ii) Kuondolewa kwenye Utumishi wa Umma kinyume na Sheria; na

(iii) Kusitishwa kwa ajira kinyume na Sheria.

Aidha, katika mkutano huo, Warufani **24** na Warufaniwa **wanne (4)** waliomba na kuruhusiwa kufika mbele ya Tume kutoa

ufafanuzi wa ziada kuhusu hoja zao za Rufaa zilizowasilishwa Tume. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 62(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022.

Vile vile, jumla ya Mamlaka za Nidhamu **tano (5)** ziliitwa mbele ya Tume kwa mujibu wa Kifungu cha 12(1)(g) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 [Marejeo ya Mwaka 2023] kwa ajili ya kutoa maelezo kutokana na kutotekeleza maagizo ya Tume yaliyotolewa katika mikutano yake iliyopita.

Katika kutekeleza jukumu la urekebu, Tume ilifanya ziara za kikazi katika Taasisi za Serikali **tano (5)** zilizopo katika Manispaa ya Morogoro ambazo ni Bodi ya Tumbaku Tanzania (TTB), Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA), Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) na Taasisi ya Utafiti wa Misitu (TAFORI). Lengo la ziara hizo lilikuwa ni kutoa elimu kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu kuhusu uzingatiaji Sheria, Kanuni na Taratibu katika Usimamizi na uendeshaji wa Masuala ya Rasilimali Watu. Vievile, Tume ilipata fursa ya kutoa elimu kwa Watumishi katika Taasisi hizo kuhusu Haki na Wajibu wao katika kutekeleza majukumu yao katika Utumishi wa Umma.

Pia, katika Mkutano huo, Tume ilipitia Taarifa mbalimbali za Utekelezaji wa Majukumu yake katika kipindi cha Robo ya

Kwanza (Julai – Septemba, 2025) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Tume inaendelea kutoa wito na kuwakumbusha Watumishi wa Umma, Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu katika Utumishi Umma kuhusu mambo yafuatayo:-

(a) Watumishi wa Umma wote kuzingatia Sheria na maadili ya kazi zao wakati wa kutekeleza majukumu yao ili kujiepusha na vitendo vinavyoashiria ukiukwaji wa Sheria na Maadili, hali inayoweza kusababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu au za kijinai.

(b) Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu katika Utumishi wa Umma:-

  (i) Kuendelea kuzingatia Sheria wakati wa kushughulikia Masuala ya Ajira na Mashauri ya Nidhamu ya Watumishi ili haki si tu itendeke, bali ionekane inatendeka.

  (ii) Kuwasilisha Tume kwa wakati vielelezo vya rufaa na malalamiko ya watumishi wanaopinga uamuzi dhidi yao.

  (iii) Kuhakikisha Taarifa za kiutumishi za kila Robo Mwaka zinawasilishwa Tume kwa wakati kama Mwongozo wa Uwasilishaji wa Taarifa

unavyoelekeza kuwa taarifa hizi ziifikie Tume ndani ya siku 30 baada ya Robo husika kukamilika.

(iv) Kutekeleza maagizo ya Tume kwa wakati badala ya kusubiri kuitwa mbele ya Tume ndipo zitekeleze maagizo hayo.

*Imetolewa Na;*

John C. Mbisso
**KAIMU KATIBU**
**TUME YA UTUMISHI WA UMMA**

23/12/2025